

**MKATABA WA KUUZA JENGO LA UKUMBI LILILOPO KUNDUCHI SALASALA
PLOTS NAMBA 2047 & 2049**

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 09 mwezi 12 mwaka 20 23 hapa Jijini
Dar es Salaam, Tanzania.

Mkataba huu unahusisha pande mbili zifuatazo:

NYAMBARI CHACHA MARIBA NYANGWINE wa S.L.P 79886, Dar es Salaam, Tanzania, Mtaa wa Jogoo Mbezi Juu, Wilaya ya Kinondoni; Mkoa wa Dar es Salaam. Barua pepe: mnyambari@yahoo.com, Simu: +255 754 959500, ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **MNUNUZI**.

na

NDUGU JOSEPHAT SIMON MAKONDA mwenye **PASI YA KUSAFIRIA (PASSPORT) na. TAE 147234, KITAMBULISHO CHA TAIFA (NIDA) Na. 19681123-14130-00001- 23** wa S.L.P 34439, Dar es Salaam; Simu +255 743 826025, barua pepe: ulakomaye@yahoo.com ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **MUUZAJI**.

Makubaliano katika mkataba huu yatazingatia sheria za **Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**.

Makubaliano maalumu ya mkataba huu ni kama ifuatavyo:-

1. **MUUZAJI** amekubali kumuuzia **MNUNUZI** jengo lililoko katika plots namba 2047 na 2049 kwa thamani ya **Tsh 650,000,000/=** (milioni miasita hamsini) tu.
2. Malipo ya kununua plots hizo yatafanyika katika awamu nne (4) kama ifuatavyo:
 - (i) Awamu ya kwanza **Tsh 35,000,000/=** (milioni thelathini na tano) tu yatafanyika tarehe 09/12/2023 kwa hundi namba **001608** ya **CRDB Bank**. Malipo haya ni kwa ajili ya kuwatoa wapangaji wote walioko katika jengo hilo
 - (ii) Awamu ya pili ni malipo ya **Tsh 65,000,000/=** (milioni sitini na tano) tu yatafanyika tarehe 19/12/2023 na siku hiyo hiyo **MUUZAJI** atamkabidhi **MNUNUZI** jengo hilo kwa ajili ya matumizi yake.
 - (iii) Awamu ya tatu ya malipo ni **Tsh 325,000,000/=** (milioni miasita ishirini na tano) tu. Malipo haya yatafanyika mara tu baada ya kukamilisha hati zote mbili toka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Pesa hizi zitalipwa na **BENKI YA FIRST HOSUING** kwa niaba ya **MNUNUZI**.
 - (iv) Awamu ya nne ya malipo na ya mwisho ni tarehe 3/01/2024. Malipo haya ni **Tsh 225,000,000/=** (milioni miambili ishirini na tano) tu. Malipo haya yatafanyika kupitia **BENKI YA FIRST HOUSING**. **MNUNUZI** ataweka fedha hizo katika **BENKI YA FIRST HOUSING** na benki hiyo watamlipa **MUUZAJI** kiasi hicho cha fedha. Makato yoyote ya nauli au fedha atakayokuwa amechukua **MUUZAJI** itakatwa baada ya majadiliano.
3. **MUUZAJI** atahakikisha kuwa amekamilisha usajili wa **HATI** katika plots zote mbili yaani plot namba 2047 na plot namba 2049 ndani ya siku 30 (thelathini) kuanzia leo tarehe 09/12/2023.

4. Mke wa **MUUZAJI** aitwaje Julieth Francis Mulanja aliyeko nchini Marekani atatuma vielelezo vifuatavyo kabla ya malipo ya awamu ya pili ya Tsh 65,000,000/= kufanyika. Vielelezo hivyo ni kama ifuatavyo:
 - Copy ya Pasi ya kusafiria yake.
 - Copy ya kitambulisho chake cha Taifa (NIDA)
 - Power of attorney kwa ajili ya kumuidhinisha binti yake kusaini mkataba huu kwa niaba yake.
 - Barua yenye picha yake ya kukubali kuuzwa kwa jingo hilo.
 - Vielelezo vingine muhimu visivyotiliwa shaka.
5. Suala la uaminifu katika biashara hii kwa pande zote mbili yaani **MUUZAJI** na **MNUNUZI** ni muhimu sana na ikiwa upande mmoja utaenda kinyume na makubaliano / masharti haya, atahitajika msuluhishi na ikiwa msuluhishi atashindwa, basi sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zitatumika ikiwa ni kwenda mahakamani.
6. Ikiwa **MNUNUZI** atashindwa kukamilisha malipo tajwa yote hapo juu hadi ifikapo tarehe 20/02/2024, **MUUZAJI** atakuwa na haki ya kutafuta mteja mwingine na kuuza jengo hilo na kumrudishia **MNUNUZI** kiasi chote cha fedha alizotoa.

JINA LA MUUZAJI:

Josephat Simon Makonda

SAHIHI:

[Signature]

TAREHE:

09/12/2023

JINA LA SHAHIDI WA MUUZAJI:

JANETH JOSEPHAT MAKONDA

SAHIHI:

[Signature]

TAREHE:

09/12/2023

JINA LA MNUNUZI:

Nyamboni Chacha Mariba Nyanguine

SAHIHI:

[Signature]

TAREHE:

09/12/2023

JINA LA SHAHIDI WA MNUNUZI:

MUHSIN ISMAIL MBAYATI

SAHIHI:

[Signature]

TAREHE:

09/12/2023

Makubaliano haya yamefanyika leo tarehe 09 Mwezi 12 Mwaka 2023

na kushuhudiwa mbele yangu

Jina:

[Signature]

Wadhifa:

Tarehe

Sahihi



[Signature]

[Signature]

[Signature]